

## TUNGO ZA KUJIBIZANA: "KUAMBIZANA NI SIFA YA KUPENDANA"<sup>1</sup>

RIDDER SAMSOM

---

Different labels have been used for marking the reciprocity in Swahili dialogue poetry, varying between the more neutral 'malumbano' or 'kujibizana' and the more marked 'ukinzani' or 'mashindano'. By showing a sample from the Zanzibari newspaper *Mwongozi* (1956) of a poetic dialogue on wife-husband relationships, the paper argues that the poetical form and the strong language used are not a mere expression of what has been called 'rivalry', but instruments in expressing views and opinions that have been observed in other literary devices (mithali, misemo, vijembe) and their usage. At the same time it is demonstrated that different types of poems (tenzi, mashairi, nyimbo) and different styles (plain, metaphoric, riddle) are used side by side. The ambiguity, incompleteness and strength of the language that is used in this poetry, make it all possible to express views on sensitive issues in the society.

---

Maneno ya sentensi hii '*kuambizana ni sifa ya kupendana*' yangeweza kuwa maneno yaliyoandikwa kwenye kanga (au watu wengine huiita lesa), bali ni jina la utenzi mfupi uliokuwa wa sita katika mfululizo wa tenzi kama kumi hivi. Hizo zimetoka katika gazeti la *Mwongozi* huko Zanzibar kuanzia tarehe 25 Mei 1956 na kuendelea hadi mwezi wa kumi na moja wa mwaka ule ule. Tenzi zote hizi zilihusu swala la uhusiano baina ya wake na waume zao. Zilikuwa zimetungwa na wanawake na wanaume pia.

Kabla sijaanza kuchambua hizo tenzi zenyewe, nataka kwanza nionyeshe 'kuambizana' huku kuna maana gani katika jamii na fasihi ya Kiswahili, kwani 'kuambizana' ni 'kupeana shauri', yaani kuambiana kwenye madhumuni maalum.

Ufasaha wa lugha ni jambo muhimu katika ustaarabu wa Kiswahili. Wasomi wengi waliochambua na kutafiti jamii hii husisitiza umuhimu huu wa kuweza kutumia lugha isiwe chombo cha mawasilano tu, bali itumike kwa ustadi na ubingwa. Mtu mwenye ufasaha na usanifu wa lugha huheshimwa na si rahisi kupewa hadhi au cheo bila kuwa na ustadi wa lugha. Ustadi huo si wa kutunga au kubuni tu, bali pia ni ustadi wa kutumia lugha fasaha kila panapohitajika. Matumizi ya lugha fasaha inayofaa muktadha (yaani 'context') fulani yamesababisha kuwepo fani mbalimbali za fasihi au, tuseme, ustaarabu au utamaduni wa lugha, kama vile **mithali**, **vitandawili**, **vijembe**, **nyimbo**, **matumizi ya lugha kwenye kanga**, na **aina za ushairi**. Fani hizo nilizotaja, ingawa zinatofautiana kifasihi, zinalingana katika jambo moja: hutumiwa na wasemaji katika hali ya aina ya mashindano. Maana, kwa kutumia **mithali** mtu hutaka kuisitiza msimamo wake kwa usemi mfupi unaokubalika na jamii yote; kwa **kitandawili** kuna mashindano ya 'kufunga na kufungua mnyama'; **vijembe** vinawakata wazungumzaji kama kisu; **nyimbo**, hasa nyimbo za taarab au nyimbo za harusi, mara nyingi

---

<sup>1</sup> Shukrani zangu ziwaendee Hamad B Mshindo (Zanzibar) na Sauda A.I Barwani (Hamburg) kwa ushauri wao kuhusu matumizi ya lugha

husikika katika hali ya mashindano fulani; kanga zenye misemo yake huenda ni jawabu fulani katika hali watu wanayoshindania.

Aina moja ya ushairi hujulikana kama 'malumbano', pengine huitwa 'kujibizana', kwa Kiingereza wasomi wengi hutumia 'dialogue verse'. Hadi sasa vimeandikwa vitabu viwili kuhusu ushairi huo wa kujibizana. Kimoja ni kitabu cha Ibrahim Noor Sharif ambacho kilikuwa shahada yake ya uzamili (PhD) 'The Function of Dialogue Poetry in Swahili Society' (1983). Cha pili ambacho mwandishi wake ni Assibi A. Amidu kinahusu aina maalum ya ushairi wa kujibizana huko Lamu inayoitwa 'Kimwondo' (1990). Naye Shaaban Robert katika 'Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini' aliandika insha 'Ukinzani' ambayo ndani yake alitaja baadhi ya mashairi yaliyotokea gazetini yakitetea shairi lake 'Ujane'.

Madhumuni ya makala hii ni kutoa mfano wa ushairi wa kujibizana na kutazama hayo mashindano ambayo yameitwa 'rivalry' na Harries (1966) na wengine, yana maana gani na iwapo kweli ni mashindano au la.

Sasa tutazame tungo zenyewe. Wa kwanza ulitokea katika gazeti la Mwongozi la tarehe 25 Mei 1956 (taz NYONGEZA mwishoni mwa makala hii). Utenzi mfupi huu una beti 20 na kutiwa saina kwa jina la Al-Mukhlisa. Hilo jina ni jina la ushairi au jina la kujificha nalo, maana yake inatokana na neno la Kiarabu 'mukhlis', yaani mwaminifu, mtu mwenye moyo safi na msema kweli pia. Kwa sababu ya mnyambuliko wa mwisho wa jina hilo Al-Mukhlisa, tunajua mtu huyu ni mwanamke, na haya yamethibitishwa pia na jina la utenzi wenyewe, kwani juu yake imeandikwa 'Wanawake Tufanyeje?'. Maudhui ('content') yake, yaani kiini cha ujumbe wake umeelezwa wazi kabisa katika ubeti kwa kwanza ambao ni:

- (1) *Bismillahi awali*                      *nanena yangu kauli*  
*Waume wenye akili*                      *wameihama dunia*

Halafu mshairi anaeleza kwa nini anawaona waume wametokwa na akili: hawashughulikii wake zao, hawajali ndoa, hawawapi wanayohitaji kwa malezi ya watoto, mavazi, na pesa. Wakati wa Ramadhani ni wakali na kutofuata sharia za kutoa zaka:

- (4) *Nyumba wanazipuuzza*              *wake wanawachagiza*  
*Hawawezi kutimiza*                      *ahadi walizotoa*

Kwa upande wa wake haiwasaidii kulalamika Wanawake wakisema au wakinyamaza mambo ni yale yale, hutolewa ukali tu, hukimbiwa nyumbani kwao, waume 'hugeuka vipepeo, kuruka wakakimbica'. Na ikiwa wanawake wanalalamika mno, mara moja hupewa talaka na hata baadaye kutopata haki zao pamoja na watoto:

- (16) *Mtoto hutoka jasho*                      *akenda kutaka posho*  
*Njoo leo njoo kesho*                      *huzungushwa kama pia*

Kwa jumla mshairi anasema kwamba hayasemekwa kwa kiasi gani wanawake walivyo na dhiki na kujuta kuolewa. Mshairi anajiuliza maswali mawili. La kwanza ni jina lenyewe la utenzi, 'Wanawake tufanyeje?', na linajibika katika mwisho wa utenzi: tujiombe Mungu atusaidie na tuwe na subira. Swali la pili analojiuliza mshairi ni kwa nini hao waume huwatendea wake zao

hivyo. Hapa ndipo katika utenzi anapowasemesha wanaume na mwenyewe kukataa kujibu swali hilo:

- (7) *Lipi linawakimbiza waume wetu nawaza*  
*Wake wanawaliwaza nyumbani mkiingia*

Lugha anayotumia si ngumu wala yenye tashbiha ('simile') na sitiari ('metaphor') nyingi au mafumbo ambayo yanahitaji werevu mkubwa wa kuyafumbua. Hata hivyo mara nyengine anatomia picha fulani kuelezea tabia ya mtu, kwa mfano anawaita wanaume 'vipepeo', au misemo kadhaa kama vile 'kuihama dunia', 'kuwatupa mbali', 'hawajali wala hawabali', 'kutoka jasho' na 'kwenda akhera'. Msamiati si ngumu pia, huenda anatia maneno yenye asili ya Kiarabu, k.m. 'nikaha' kwa ndoa au 'kuwadia' kwa kufika, lakini maneno kama hayo ni maneno ya msamiati wa msingi wa Kiswahili kinachosemwa Zanzibar. Mara moja tu anabuni neno jipya ambalo maana yake inaeleweka kutokana na msingi, muktadha na vina vyake: ubabazi, yaani ubabaifu. Hata hivyo neno hili linaweza kuwa limekosewa tu katika uchapishaji, kwani neno 'ubabazi' lingefaa kabisa katika muktadha huu:

- (11) *Kifika mwisho wa mwezi hujitia ubabazi*  
*Waume hawasikizi lo lote utawambia*

Ingawa tungo nyingi zilizotoka katika gazeti ni za aina ya shairi, utungo huu ulitungwa katika umbo la utenzi: yaani ubeti mmoja una mishororo miwili yenye mizani 16. Mishororo hiyo ina vina vitatu, kati na mwisho wa mishororo wa kwanza na kati ya mishororo wa pili. Kila irabu ya mizani ya mwisho wa ubeti ina vina katika beti zote. Kila mishororo una mizani 16. Uchambuzi na istilahi hizi zinatokana na Ibrahim Noor Sharif (1958:51). Kaluta Amri Abedi huchambua utungo wa utenzi kwa namna nyengine: 'ni ushairi wenye mizani chache kuliko 12, ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mistari, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mistari wa mwisho katika kila ubeti, ambao huendelea na kina cha namna moja kinachoitwa bahari. Tenzi nyingi zaidi huwa zenye mistari mine na mizani minane' (1954:29). Tenzi tunazozungumzia hapa zinafuata uchambuzi wa Kaluta Amri Abedi kwa vile zimechapishwa gazetini zenye mistari mine. Bila shaka uchambuzi wa Ibrahim Noor Sharif unatokana na arudhi ('prosody') ya tenzi zinapoimbwa. Uchambuzi wake unahusiana na sauti za tungo, sauti za ngoma na mahadhi ('melody') yake. Inavyoonekana tofauti kati ya wasomi hao wawili inatokana na tofauti kati ya fasihi inayoandikwa na kusomeka tu na fasihi inayoimbwa na kusikika. Basi, suala hilo haliwezi kutatuliwa hapa kwani vipi tujue nini inatokea kichwani au moyoni mwa msomaji au mtungaji anaposoma au kutunga utungo fulani: husoma tu au anasikia na kuimba vile vile?

Utenzi huu '*Wanawake tufanyeje*' ulitaka jawabu na kweli jawabu zilikuwa zikiingia ofisini kwa wahariri wa gazeti la Mwongozi. Baada ya wiki tatu, yaani tarehe 15 Juni, tenzi mbili zilichapishwa kwenye ukurasa wa sita. Mmoja ulitungwa na mwanamme kutoka Pemba aitwaye Salum Muhammed Khamis Sheibany, mwengine na mwanamke aliyelitwa Moza Ali kutoka Zanzibar. Utenzi wa kwanza unaitwa '*Bora Msingalisema*' na una beti 17. Msimamo wa mshairi Salum Muhammed unadhihirika mara katika mwanzo wa utenzi wake. Baada ya ubeti wa kwanza:

- (1) *Naanza Bismi-lahi natunga nikifurahi*  
*Kukujibu nitawahi Bintil-Mukhlisa*

anaendelea:

- (2) *Hayo uliyoyanena si makosa ya mabwana*  
*Bali nanyi kina mama upenzini kujitoa*

Anaeleza kwamba si kwa sababu ya waume ndoa kuharibika, bali wanawake, wao ndio chanzo cha balaa zote. Wana majivuno, wanawajibu waume zao kwa ujeuri, wenyewe wamejitoa upenzini. Wanaume hujitahidi ndoa kufanikiwa, huchapa kazi kupata rizki yao, wengine wanabaki maskini ingawa wako njiani tu wapate chochote. Lakini hizo jitihada zote za bure tu, kwani:

- (9) *Unaporudi nyumbani kuitia kitu tumboni*  
*Bibi yupo mlangoni wima kakusimamia*

- (10) *Hapo utamnasihni kumuuliza asahi*  
*Ni nini cha ikrahi kwako kilo kutokea*

Hatimaye mshairi anaishia utenzi wake kwa kuwaombea wanawake dua na kuwapa mawaidha:

- (17) *Tujalie kupendana kwa mabibi na mabwana*  
*Wazee na wao wana Isilamu wote pia*

Katika kumjibu Al-Mukhlisa mshairi anatumia dhana nyingi zilizokuwa zimetumika katika utenzi anaajibua: haja ya kutimiza ahadi, kukumbuka sharia, kuwepo njiani, kuwepo kwa balaa, kuzingatia fikra. Analinganisha shida kati ya mke na mume na ndwele, neno la Kipemba na Kimvita ambalo maana yake ni maradhi. Lakini kama Mukhlisa mwenyewe, Salum Muhammed pia hajui sababu ya hayo yote, ila tu kujitoa kwa wanawake upenzini:

- (11) *Hutatambua asili tadhani ni radi kali*  
*Kukujibu kwa fedhuli mwisho utajichukia*

Jawabu la pili ni utenzi wenye beti 10 wa Moza Ali. Huyo alikuwa ni mshairi aliyejulikana sana huko Zanzibar wakati wa harakati za kupigania uhuru. Kati ya mwaka 1952 na 1964 zaidi ya tungo zake 80 zilikuwa zimechapishwa katika gazeti la Mwongozi. Jan Knappert alichapisha utenzi wake wa abjadi 'Adhabu za Jahannamu' katika jarida la "Swahili Journal" (1964). Nao akina Sengo wamewahi kuhariri mashairi yake machache katika 'Mashairi ya Mfungo wa Ramadhani' (1979). Sauda Sheikh na Eleonore Adwiraah walitoa mashairi matatu na habari za maisha yake katika 'Moza Ali, eine Dichterin aus Zanzibar' (1983). Ametajwa pia katika 'History of Kiswahili Poetry [A.D. 1000-2000]' waliyofanya I.S.Y. Sengo na M.M. Mulokozi (1995). Washairi 29 wa Pemba na Unguja walipoulizwa nao, ni nani mshairi mwanamke ambaye kazi yake wanaipenda hasa, walikuwa wakimweka Siti binti Saad awe wa kwanza naye Moza Ali wa pili (Uk 84).

Wakati alipotunga utenzi huu mfupi ulio na beti kumi tu, alikuwa na umri wa miaka ishirini na moja. Aliuita 'Mukhlisa nakuwasa'. Lakini hamwonyi Mukhlisa tu na *kumwambia 'kwani umekosa sana kuwatukana mabwana'*, bali anawataja watu wengine watatu. Mmoja wao

anamtolea mwito kuwanyamazisha wengine; wawili wengine anawalaumu kwa kuingilia kwa 'ukali' na kwa 'vigudi' na 'makeke makeke'. Inavyoelekea, gazetini zilikuwemo tungo zao kati ya utenzi wa Mukhlisa na hizo mbili za Salum Muhammed na Moza Ali. Mwongozi ilikuwa ni gazeti la kila wiki. Kwa bahati mbaya matoleo mawili ya tarehe Mosi Juni na 8 Juni hayakupatikana katika Nyaraka za Zanzibar wala Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.<sup>2</sup> Hata hivyo ni dhahiri kwamba wanaume wawili wameshajibu utenzi wa Mukhlisa na, kufuatana na Moza Ali, kutunga tenzi zao zenye hamaki na ukali:

- (7) *Khasa Shekhe Aswedi*      *hamaki zimemzidi*  
*Kutujiya kwa vigudi*      *na kutukana vibaya*
- (9) *Naye Bwana El Mauli*      *mara katowa ukali*  
*Jama hayo si halali*      *ya dhara kushangiliya*

Ujumbe wa mshairi huyu una vipengele viwili. Kwanza anamwambia Mukhlisa ikiwa mwanamme mmoja anakosa, sio wote walio wabaya:

- (3) *Kama kakosa mmoja*      *sivyo wote kuwafuja*  
*Mambo huwenda kwa daraja ya kufuata shariya*

Pili anatoa kauli na mawaidha:

- (4) *Sikiza yangu kauli*      *aso hili ana hili*  
*Nisai na marijali*      *wako wema na wabaya*

Kwa kweli suluhisho lake la kutatua matatizo hayo ya ndoa ni sawa sawa na suluhisho la Mukhlisa:

- (5) *Inapasa kusubiri*      *asa itakuwa kheri*  
*Na alofikwa na shari*      *Rabi atamwondosheya*

Naye Sheykha Bint Sheikh wa Kilifi huko Kenya pia anatoa mawaidha hayo gazetini humo, mnamo 22 Juni, 1956, wiki moja baadaye:

- (14a) *Ilobaki kusubiri*      *na kushukuru Jabari*

lakini hayo ni shtihizai ('irony') tu, kwani katika ubeti ule ule anaendela kuwaonya waume:

- (14b) *Takaneni muaziri*      *Mungu atatulipia*

Utenzi wake wenye beti 17 ameuita 'Waume Zingatieni, Wake Mnatuonea'. Isipokuwa anamwita Bi Moza 'Binti mwenye fahamu', kumtaka radhi na kumwomba usahibu wake, anamtetea Mukhlisa kwa moyo wote na kuwashambulia waume moja kwa moja, bila pingamizi yoyote:

- (8) *Daima mwatutukana*      *waume mkikutana*  
*Mazungumzo hamna*      *ila wake jamia*

Anawaambia wanaume waliojibu:

<sup>2</sup> Wakati wa kuhariri na kutayarisha makala hii kwa uchapishaji nimeshayapata (rhs)

- (7) *Huku si kujibishana mwataka adhiriana*  
*Ikiwa ni kutukarwa nisai tushazoea*

Jinsi walivyotaharuki anafananisha na rikodi:

- (9) *Kula siku mwaabiri ya siri na ya dhahiri*  
*Hata mwisho santuri imekwisha kutolewa*

Anaishia utenzi wake ambao haukuficha maoni yake na kuwa na lugha kali, kwa kumwomba Moza Ali usahibu wake na '*majibu kunetea*' (maana yake: kuniletea).

Basi ilichukua mpaka toleo lililofuatia la 29 Juni, jawabu ya Moza Ali kutokea Mara hii katika beti zake 11 hakumshambulia Mukhlisa tena, alionyesha huruma zake kwake na kumwelewa shida zake:

- (3) *Kwa hakika ana dhiki kwa mume kumhiliki*  
*Ndipo alipohamaki akaanza kupoteya*

Hata hivyo anarudiarudia maoni yake ya '*Mukhlisa nakuwasa*' kwa vile anaona bora kumwingilia yule tu aliyemkosa Mukhlisa na sio waume wengine ambao ni wacha Mungu. Lakini anakubaliana na Sheikh binti Sheikh kuwa:

- (8) *Walojipa uhodari kutwimba kwa santuri*  
*Wao si watu wazuri bora kuwanyamazia*

Na ndivyo anavyojaribu mwishowe katika utenzi wake, kuutuliza ugomvi uliotokea katika majadiliano yote:

- (10) *Bi Shekha kuambizana ni sifa ya kupendana*  
*Na Ilahi Subhana sana ametuusiya*

Basi, majadiliano yalitulia kidogo kwa muda wa wiki saba mpaka katika matoleo ya tarehe 17 na 24 Agosti utungo wenye beti 35 ulichapishwa katika sehemu mbili. Haukuwa utenzi tena, mara hii ilikuwa katika umbo la nyimbo (mishororo mitatu). Mshairi anajiita kwa jina la kuwatisha watu Ibni Sharri Anamtetea Mukhlisa sana, kumwita '*mwanangu*' na kusema kuhusu waume:

- (2) *Si haki waliotenda naona wamuonea*  
*Nawaacha wataranda hasema watamwachia*  
*Naona mambo yapanda bora naona kungiya*

Sehemu kubwa ya nyimbo yake yenye jina '*Mwanangu kumuonea hadi naumia sana*' inaeleza kisa kirefu kuhusu mwanamme mmoja aliyeibiwa pesa na kijana mmoja aliyekuwa karibu naye Kwa kweli, kisa hiki kinaweza kikawa ni fumbo. Inategemea msikilizaji anataka kuelewa vipi na kufumbua kwa namna gani: inaelekea hizo pesa si pesa bali ni mkewe. Lakini huyu aliyeibiwa yumkini ana mpenzi pia. Kwa kweli, ni mafumbo, yaani Ibni Sharri anataka kuwaambia watu kuwa wanawake kwa wanaume wakigombana ni kwa sababu wana wapenzi? Hatujui, lakini tunayojua ni utetezi wake wa Mukhlisa:

- (20) *Binti Mukhulisiya mwanangu nimpandaye*  
*kwa hapa nampa njiya neno baya awambiye*  
*Na kama yawachukiya hapo ni nyinyi na miye*

Al Mukhlisa anajibu tarehe 7 Septemba. Hagusi tena mada ya wake kuonewa na waume. Anamshukuru tu na kumkarabisha Ibnī Sharri, ambaya anamwita 'Mpenzi Baba Yangu'.

- (2) *Zako nyingi shukrani*      *kwa wema na ihsani*  
*Kuja ukaniauni*              *vita vilipozongea*

Anatubu kwa kuanzisha hivi vita na kujitetea:

- (18) *Nasaha nilisikiza*              *nikakaa kanyamaza*  
*Hufikiri nikiwaza*              *mbona wananionea*

Baada ya jawabu hii ya Mukhlisa bado tungo ziliendelea kuingia na kuchapishwa. Nayataja tu majina yao (pamoja na tarehe):

- 21 Septemba: '*Ukisema Ukisaza, Yangu Ninakuusiya*'  
 12 Oktoba: '*Ni Bora Ukatuliya, Sijitiye Mshawasha*'  
 19 Oktoba: '*Msitafute Udhiya, Nawawasa Nyamazeni*'  
 2 Novemba: '*Ilahi Rabana, Tanihukumia*'

Nini imetokea katika tungo zote hizo za kujibizana? Kwanza mshairi mmoja aliyejiita Al-Mukhlisa ametupa chambo na kutazama samaki gani watakuja kutafuna. Ndoana ilikuwa ni kali sana Aliyozungumzia, wake kuonewa na waume, ni yale yaliyowafikia wanawake wengi na kujadiliwa sana wakati ule huko Zanzibar, kama ilivyoonekana pia katika makala mbalimbali zilizotokea katika gazeti lile lile. Kati ya samaki waliokuja kutafuna chambo, Bi Moza Ali anachukua nafasi muhimu. Si kwa sababu ya tenzi zake tu na siasa yake kuwaelekea wanaume kwa wanawake wanaojibizana, lakini pia kwa vile wengine wanavyomtaja na kumsemesha. Katika kujibizana yeye akawa muhimu kuliko Mukhlisa mwenyewe kwa kiasi ambacho tunajiuliza kuwa, huyo siye Mukhlisa mwenyewe? Si mtindo tu anavyotunga Mukhlisa ambao unatudhanisha ndiye. Vile vile mwenyewe Bi Moza anatoa ushahidi kidogo mara ya kwanza anapoingia katika kujibizana kwa kumwambia Shekh Awsedi: '*umetujia kwa vigudi*' Yumkini anachukua nafasi ya wake kwa jumla, lakini katika utenzi wake mwengine anamwambia Sheikha binti Shekh: '*Mukhlisa ni mwenzangu, lake yeye ndilo langu*'. Ikiwa kweli kama tunavyofikiri Bi Moza mwenyewe ndiye chanzo cha majadiliano, basi mashindano hayo si kwa ajili ya kushindana tu, lakini ni njia au, tuseme, mtindo wa kuwekea dhamira ('theme') jukwaani kwa jamii.

Katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili wasomi kadhaa wamejaribu aina mbalimbali za matumizi ya tungo ziunganishwe na mada zinazozungumziwa katika hizo tungo. Ibrahim Noor Shariff (1983) amesainisha namna tano za matumizi: tungo za maoni ya kifalsafa, za kuhadithia, za mafunzo, za dua na za mawasiliano. Lakini katika mfano wetu mmoja tu wa kujibizana tumeona kwamba mambo hayo yote matano yamo: maoni, kisa, mafunzo, dua na mawasiliano.

Wasomi wengi wengine wamejaribu arudhi mbalimbali za tungo ziwe zihusiane na yaliyomo katika tungo au lengo lake. Wanaeleza kwamba tenzi zingefaa dini na hadithi refu, mashairi yangetumika kwa siasa au mawasiliano, nyimbo ziwe kwa harusi au ngoma. Hapa tumeonyesha kuwa fani mbalimbali za arudhi zimetumika kwa kujibizana. Vile vile mitindo mbalimbali ya kifasahi inavyochambuliwa na Ibrahim Noor Shariff inatumika yote pamoja wakati mmoja:

mtindo wa moja kwa moja ('plain style'), tashbiha ('simile') na sitiari ('metaphoric style'), na mafumbo ('riddle style').

Katika makala yake kuhusu vijembe kwenye kanga 'The Power of Incompleteness: innuendo in Swahili women's dress' (1996), David Parkin anajiuliza kwa nini aina ya matumizi ya lugha kama hii ina nguvu sana. Mtu akitaka mwenzake kumsikiliza hatumii lugha ya kila siku. Akitaka kumshawishi mtu au kusisitiza jambo fulani hutumia lugha maalum yenye mitindo maalum, hutumia lugha yenye nguvu. Anasema Parkin: 'Perhaps it can be suggested that the "violent" uses of innuendo most likely typify rhetorical persuasion and the more pacific and evocative uses inform poetics. But even this comes close to yet another dangerous tautology and one suspects that the problem here is, indeed, that rhetoric and poetics have been defined as separate discourses rather than as arbitrarily defined bundles of overlapping tendencies within discourse' Ushairi wa kujibizana unaonyesha hayo matumizi maalum makali ya lugha yanavyotumika pia katika vijembe. Madhumuni yake ni haja ya kutaka kushawishi, ushawishi ('persuasiveness'). Lakini mashindano hayo si kushindana, bali ni kuwasiliana, kulumbana, kujadiliana pamoja na kukinzana. Ni kuambizana, na, asemavyo Moza Ali, ni kupendana.

#### MAREJEO

- Assibu A. Amidu. 1990 *Kimwondo: A Kiswahili electoral contest*. Wien: Beiträge zur Afrikanistik.
- K. Amri Abedi. 1954 [repr. 1979]. *Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Harries, Lyndon. 1963. *Swahili poetry*. Oxford: Clarendon Press.
- Harries, Lyndon. 1966. *Poems from Kenya: Gnostic verses in Swahili by Ahmad Nassir bin Juma Bhalo*. Madison, Milwaukee, London: University of Wisconsin Press.
- Ibrahim Noor Shariff. 1983. *The function of dialogue poetry in Swahili society*. Ph.D. dissertation Rutgers University, New Jersey. Ann Arbor: University Microfilms.
- Ibrahim Noor Shariff. 1988. *Tungo zetu*. Trenton, N.J.: The Red Sea Press.
- Knappert, Jan (ed.). 1964. "Adhabu za Jahannamu". *Swahili Journal* 34,1.
- Mulokozi, M.M. and I.S.Y. Sengo. 1995. "History of Kiswahili poetry [A.D. 1000-2000]." University of Dar es Salaam: OSSREA/IKR.
- Mwongozi*. Mei - Nov 1956. Zanzibar: Ahmed S. Kharusi.
- Parkin, David. 1996. "The power of incompleteness: innuendo in Swahili women's dress." *Anthropologie de l'interlocution*. ed. by B. Masquelier and Jean-Louis Siran. Paris: l'Harmattan. [Forthcoming].
- Shaaban Robert. 1991 [repr.]. *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.



NYONGEZA: kutoka gazeti la Mwongozi Vol 15 No 17, p 6, 25 Mei 1956

WANAWAKE TUFANYEJE ?

- |     |  |   |
|-----|--|---|
| 1.  | Bismillahi awali<br>Waume wenye akili      | nanena yangu kauli<br>wameihama dunia       |
| 2.  | Wameihama dunia<br>Hapa waliobakia         | Wanaojua sharia<br>ni wengi wenye udhiya    |
| 3.  | Sharia hawaijali<br>Wake wawatupa mbali    | nikaha hawaibali<br>waandama yao njia       |
| 4.  | Nyumba wanazipuza<br>Hawawezi kutimiza     | wake wanawachagiza<br>ahadi walizotoa       |
| 5.  | Wake wakizaa nao<br>Kwa jina si kwa kivao  | watoto huwa ni wao<br>wala si kwa kutumia   |
| 6.  | Hasa waume wa leo<br>Hugeuka vipepeo       | ati hata wenye cheo<br>kuruka wakakimbia    |
| 7.  | Lipi linowakimbiza<br>Wake wanawaliwaza    | waume wetu nawaza<br>nyumbani mkiingia      |
| 8.  | Majibu yatushangaza<br>Ni haki kutekeleza  | jambo linowakimbiza<br>na kukabili sharia   |
| 9.  | Wanawake masikini<br>Wajitahidi yakini     | wametuliza makini<br>yao yawaendea          |
| 10. | Kwani huitafuta kazi<br>Wakawalipa walezi  | wakajivisha kivazi<br>na watoto wao pia     |
| 11. | Kifika mwisho wa mwezi<br>Waume hawasikizi | hujitia ubabazi<br>lo lote utowambia        |
| 12. | Ramadhani 'kiwadia<br>Huna la kuwaambia    | ukali wanajitia<br>wakaibadili nia          |
| 13. | Sikukuu jambo moja<br>Watatoa kila hoja    | Zakaa inawangoja<br>ya kukimbia sharia      |
| 14. | Wake wakilalamika<br>Watoto na kuwataka    | maia wapewa talaka<br>kama waliwalipia      |
| 15. | Wakiwacha wake zao<br>Husahau haki zao     | pamoja na wana wao<br>watoto kuwangilia     |
| 16. | Mtoto hutoka jasho<br>Njoo leo njoo kesho  | akenda kutaka posho<br>huzungushwa kama pia |
| 17. | Wake wanaponyamaa<br>Wakinena huwa baa     | waume huchachawaa<br>mpaka kupindukia       |

- |     |   |  |
|-----|---|--|
| 18. | Mradi hayasemeki<br>Wanawake wana dhiki | waume wanahiliki<br>wanajuta kuolewa   |
| 19. | Sasa yaliyobakia<br>Mungu tatusaidia    | ni duwa kujiombea<br>tuzidi kuzingatia |
| 20. | Iuwe wana wa subira<br>Mola atupe ijara | tukenda kesho akhera<br>aliyotuandikia |
- Al-Mukhlisa